# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara yaChukwani, Buyu,
70490 MjiniMagharibi,
S.L.P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 2242000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA UTALII, BIASHARA NA KILIMO YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,**

Awali ya yote, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi mungu Mtukufu, mwenye kustahiki kushukuriwa na Viumbe vyote kwa kutujaalia uhai na afya njema tukaweza kukutana katika Baraza hili Tukufu kwa lengo la kuendelea kuwatumikia Wananchi wa Zanzibar kwa kutekeleza majukumu yetu mbali mbali kwa niaba yao ambapo leo tupo hapa kuipitia na kuijadili Bajeti ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Namuomba Mwenyezi Mungu anijaaliye ufasaha katika uwasilishaji wa Hotuba hii na atupe usikivu na uelewa ili hatimaye tuweze kuichangia kwa umakini bajeti hii kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**

Tunatoa pongezi za dhati kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa

uongozi wake uliotukuka unaopelekea kuendelea kuimarika sekta mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha uchumi wa nchi yetu. Aidha, niwapongeze pia wasaidizi wake wa karibu Makamo wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamu wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah kwa namna wanavyojitolea kwa moyo wao wote katika kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kufanikisha malengo ya nchi yetu tuliyojiwekea.

**Mheshimiwa Spika,**

Tunatoa pongezi maalum kwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi Mheshimiwa Shaaban Ali Othman kwa uongozi wake imara ambao umewafanya watendaji wote wa Wizara hii kuanzia Katibu Mkuu Kepteni Hamad Bakari Hamad, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Zahor Kassim Mohammed pamoja na watendaji wao wote kwa mashirikiano mazuri yaliyoiwezesha Kamati yetu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. Ni imani yetu kuwa, mashirikiano baina yetu yatazidi kuimarika siku hadi siku na kuleta wepesi wa kutekeleza majukumu yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba sasa niwatambulishe Wajumbe wa Baraza lako Tukufu Wajumbe wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa kuwataja kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Mwenyekiti
2. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Said Saleh Salim - Mjumbe
4. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Mjumbe

5. Mhe. Mihayo Juma Suleiman - Mjumbe
6. Mhe. Dkt. Mohammed Ali Suleiman - Mjumbe
7. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis - Mjumbe
8. Mhe. Suleiman Makame Ali - Mjumbe

Aidha, Kamati inafanya kazi kwa kushirikiana na makatibu watatu na msaidizi mmoja ambao ni:

1. Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi - Katibu
2. Ndg. Yussuf Mkamba Mwinyi - Katibu
3. Ndg. Asma Ali Kassim - Katibu
4. Ndg. Azmina Khamis Hamad - Msaidizi

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo imefanya kazi ya kuchambua na kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa kuzingatia matakwa ya Jadweli la Kwanza la Kanuni ya 97(1) ya kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2020 siku ya Jumanne tarehe 30 Aprili, 2024. Kimsingi, Kamati imeyapitisha makadirio hayo baada ya kufanya majadiliano na Wizara na kupendekeza marekebisho madogo madogo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa ruhusa yako, naomba sasa nitoe maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa Programu Kuu na Programu ndogo za Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ambazo Kamati imezitolea maelekezo na ushauri.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mujibu wa Bajeti inayozingatia program (PBB), Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imeundwa na Fungu Kuu moja la L02 na limepangiwa kutekeleza Programu kuu tatu (3) zenye Programu ndogo sita (6) ambazo kwa ujumla wake zinajumuisha shughuli na huduma zote zinazokusudiwa kutekelezwa  na Wizara hii, katika mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inatarajiwa kukusanya jumla ya Tsh. Bilioni 5,921,734,000 kupitia vyanzo vyake mbali mbali vya mapato. Aidha, Wizara inakadiriwa kutumia jumla ya Tsh. Bilioni 66,128,166,000. Kati ya fedha hizo Tsh. Bilioni 10,985,000,000 ni kwa ajili ya kazi za kawaida ambapo Tsh Bilioni 4,130,200,00 ni Mishahara, Tsh. Bilioni 2,501,400,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Uendeshaji wa Ofisi na Tsh Bilioni 4,353,400,000 ni Ruzuku kutoka SMZ za Wizara zinazojitegemea. Katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, Wizara imetengewa jumla ya Tsh. 55,143,166,000 ambapo Tsh. 39,000,000,000 kutoka SMZ na Tsh. 16,143,166,000 kutoka kwa washirika wa maendeleo.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU

**Mheshimiwa Spika,**

Programu Kuu hii ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu imeundwa na Programu ndogo moja ya maendeleo ya Uchumi wa Buluu na Huduma sita (6) ambazo zinatekelezwa na Idara ya Maendeleo na

Uratibu wa Uchumi wa Buluu (Pamoja na Mafuta na Gesi). Aidha, lengo kuu la Programu Kuu hii ni Kuratibu na kutekeleza masuala mtambuka yanayohusiana na Uchumi wa Buluu. Programu hii kwa mwaka wa Fedha 2024/2025, imeombewa jumla ya Tsh. bilioni 11,205,996,000 ikiwa ni upungufu wa Tsh. Bilioni 5,941,387,000 kutoka kwenye bajeti ya mwaka unaoishia June 30, 2024 ambayo ilikuwa ni Tsh. Bilioni 17,147,383,000.

**Mheshimiwa Spika,**

Upatikanaji wa uhakika wa nishati ya mafuta na gesi asilia ni nyenzo muhimu ya kufikia maendeleo endelevu ya Taifa lolote duniani. Kwa kulitambua hilo, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imetenga jumla ya Tsh. 4,000,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kuhifadhia bidhaa za petroli iliyosafishwa na usambazaji kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kamati inaunga mkono ujenzi wa kituo hicho na inaiomba Serikali kuharakisha ujenzi huo ili kuiepusha nchi yetu na janga la upungufu wa mafuta ambao tumekuwa tukiushuhudia mara kwa mara nchini unaopelekea usumbufu kwa wananchi na kudumaza shughuli za kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imefarajika sana na zoezi la utangazaji wa vitalu vipya vya uwekezaji wa utafutaji wa mafuta na gesi asilia kwa maeneo ya bahari, ambalo limefanywa kwa mashirikiano kati ya Serikali, Kampuni ya SLB pamoja na Frontier ambapo tarehe 20 Machi, 2024 uzinduzi wa zoezi hili ulifanywa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Wizara kwa kutenga jumla ya Tsh. Bilioni 4,000,000,000 kwa ajili ya kuanzisha kituo cha kuhifadhia taarifa za mafuta na gesi asilia (national data respository) ikiwa ni hatua muhimu katika uendelezaji wa sekta ya mafuta na gesi nchini. Kituo hiki kitakuwa ni sehemu muhimu inayotoa mwanga wa kiwango cha mafuta kilichopo katika eneo husika na kupelekea kuuzwa taarifa hizo kwa wawekezaji wenye nia ya kuekeza kwenye sekta hii. Tunaiomba Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuipatia fedha hizo Wizara ili kufanikisha suala la uanzishwaji wa kituo hiki kwa uendelezaji wa nishati hii muhimu.

**Mheshimiwa Spika,**

Tunatoa shukurani kwa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa kusikia kilio cha wananchi wa Ndagoni walioathirika na shughuli za utafiti wa mafuta na gesi kwa njia ya mtetemo na kuwanyamazisha kilio hicho kwa kuwapatia fidia za uharibifu wa mazao ya baharini. Kamati imeridhishwa na hatua hiyo muhimu na inaishauri Wizara kukamilisha malipo ya fidia kwa maeneo mengine yaliyobakia ili kujenga imani ya wananchi kwenye shughuli za Serikali yao.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UVUVI

**Mheshimiwa Spika,**

Programu Kuu ya Maendeleo ya Uvuvi imeundwa na Programu ndogo mbili ambazo ni Programu ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini na Programu ndogo ya Uhifadhi wa

Rasilimali za Bahari. Programu zote hizi kwa pamoja zinatekelezwa na Idara ya Uvuvi na Maendeleo ya Mazao ya Baharini pamoja na Idara ya Uhifadhi wa Bahari. Aidha, Programu Kuu hii ina lengo la kuendeleza uvuvi na kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao ya baharini kwa njia ya ufugaji. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu hii inakadiriwa kutumia jumla ya Tsh. Bilioni 51,204,682,000 katika kutekeleza shughuli mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,**

Tafiti za uvuvi na mazao ya baharini ndio dira ya kutuongoza juu ya uendelezaji wa sekta nzima ya uchumi wa buluu nchini. Kwa mnasaba huo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha Taasisi ya ZAFIRI ambayo iko chini ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa ajili ya kuendesha tafiti za kitaalamu kuhusiana na masuala ya bahari na uvuvi. Kamati iliarifiwa kuwa, hadi kufikia Aprili, 2024 tafiti mbalimbali zimefanywa na Taasisi hii kwa hatua tofauti. Tunatoa pongezi kwa Wizara na Taasisi ya utafiti ya ZAFIRI na tunaiagiza kukamilisha tafiti zinazoendelea ili tupate mwelekeo sahihi. Pia, tunaishauri Serikali yetu sikivu kuiongezea fedha Taasisi hii kwa kadri hali inavoruhusu na kuyatumia ipasavyo matokeo ya tafiti hizo katika kufanya maamuzi sahihi ya shughuli za uvuvi na matumizi ya bahari nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO) ni Taasisi iliyoundwa kwa ajili ya kuendeleza shughuli za uvuvi nchini. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Kampuni inakadiriwa kutumia jumla ya Tsh. Milioni 386,800,000 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake za msingi. Kamati imearifiwa kuwa ZAFICO imeweza kukamilisha ujenzi

kiwanda cha kusarifu dagaa katika eneo la Kama katika hatua za awali kwa asilimia 70. Aidha, kwa upande wa Pemba, mradi kama huo unaendelea baada ya kupitia changamoto katika kipindi kilichopita. Ni matumaini yetu kuwa Mkataba baina ya Serikali na mkandarasi mpya wa mradi huu Kampuni ya Lucolo Constuction Company utasainiwa na kazi itaanza kwa muda uliopangwa ili hatimaye miradi hii yende sambamba na kufunguliwa pamoja kwa Unguja na Pemba. Aidha, Kamati inaitaka Wizara kumsimamia vyema mkandarasi huyo kwa kushirikiana na Mshauri Mwelekezi ili tufikiye malengo tuliyojipangia.

**Mheshimiwa Spika,**

Huduma ya Ujenzi wa Madiko ya kisasa na masoko ya samaki (HL02020103) inakadiriwa kutumia jumla ya Tsh. Bilioni 27,000,000,000 kwa mwaka wa fedha 2024/2025, ikiwa ni ongezeko la zaidi ya asilimia 50 ya fedha zilizotengwa mwaka uliopita kwa ajili ya shughuli hii. Kamati imejionea madiko mbalimbali yaliyojengwa Unguja na Pemba na kuarifiwa juu ya changamoto za ujenzi na uendeshaji wake zinazochangiwa na mfumo wa usimamizi baina ya wananchi, Wizara ya Uchumi wa buluu na uvuvi pamoja na Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara maalum za SMZ. Hivyo, tunazishauri Taasisi mbili hizi za Serikali kuwa na mashirikiano yatakayopelekea ujenzi wa masoko na madiko katika maeneo yenye uhitaji zaidi pamoja na uendeshaji bora wa masoko na madiko hayo kwa maendeleo ya wavuvi na sekta nzima ya uvuvi nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Wizara kwa kukamilisha zoezi la ugawaji wa boti 527 za uvuvi na 500 za mwani zilizotokana na fedha za ahueni ya UVIKO 19 kwa wakulima wa mwani na wavuvi wadogo wadogo pamoja na zana zake zinazohusika ikiwemo mashine na vifaa vya kutafutia Samaki. Kwa kiasi kikubwa shughuli hii imekamilika ingawa kuna baadhi ya wanufaika wanaendelea kukamilisha taratibu ili waweze kukabidhiwa boti zao. Aidha, Kamati inaitaka Wizara kuwafuatilia wanavikundi waliopewa boti hizo kwani baadhi yao wamekua wakibadilisha matumizi ya boti hizo na kulifanya lile lengo la Serikali kushindwa kufikiwa.

**PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI**

**Mheshimiwa Spika,**

Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imeundwa na Programu ndogo Tatu, zinazojumuisha Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji, Programu ndogo ya Mipango, Sera na Tafiti na Programu ndogo ya Uratibu wa Kazi za Uchumi wa Buluu Afisi Kuu Pemba. Aidha, Programu Kuu hii inatekelezwa na Idara ya Utawala na Uendeshaji na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Lengo la programu hii ni kutoa huduma za kiofisi kwa ufanisi na ustawi kwa sekta. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu hii imekadiriwa kutumia jumla ya Tsh. Bilioni 3,717,488,000. Kamati inaiomba Serikali kuipatia Wizara fedha zitakazoidhinishwa ili kufanikisha shughuli zake.

HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda kuitanabahisha Wizara kwamba fedha ambazo Baraza lako Tukufu itaziidhinisha kwa Wizara hii ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ni fedha za walipa kodi zinazotozwa kutoka kwa Wananchi. Hivyo, Kamati yangu inaitaka Wizara kuwa makini katika matumizi itakayoyafanya ili yale malengo waliyoyapanga yaweze kufikiwa na Wananchi nao wanufaike ipasavyo kwa mrejesho utakaofanywa kwa matumizi mazuri ya fedha zao.

**Mheshimiwa Spika,**

Mwisho napenda kuwashukuru na kuwapongeza tena Viongozi na Watendaji wa Wizara hii kwa juhudi wanazochukua katika kutekeleza kazi zao pamoja na ushirikiano waliotupatia wakati wa kuipitia Bajeti yao. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa vile Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2024/2025, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waijadili na kutoa mapendekezo hayo na hatimae kuipitisha Bajeti hii ili kumruhusu Mheshimiwa Waziri kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa niaba ya Kamati yangu na wananchi wa Jimbo la Mtoni naiunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.



…………………….

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu,
Makamo Mwenyekiti,
Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**